**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA BALOZI DKT. EMMANUEL JOHN NCHIMBI, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UFUNGUZI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA MISITU DUNIANI NA KAMPENI YA UPANDAJI MITI KITAIFA

**KIWANJA CHA ILULU – LINDI**
**19 MACHI, 2026**

- ***Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), Waziri Wa Maliasili Na Utalii;***
- ***Mhe. Zainab Telack, Mkuu wa Mkoa wa Lindi, na Wahe. Wakuu wa Mikoa wote Mliopo;***
- ***Mhe. Mohamed Jarufu, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Lindi;***
- ***Mhe. Hamad Chande (Mb.), Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii;***
- ***Mhe. Timotheo Mnzava (Mb.), Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, pamoja Wahe. Wabunge wote mliopo hapa;***
- ***Dkt. Hassan Abbasi, Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii;***
- ***Mhe. Victoria Mwanziva, Mkuu wa Wilaya ya Lindi, na Wakuu wa Wilaya wote mliohudhuria;***
- ***Bi. Zuwena Omar, Katibu Tawala wa Mkoa wa Lindi, na Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya wote mlioungana nasi hapa;***
- ***Wadau wa Maendeleo mliopo;***
- ***Viongozi wa dini;***
- ***Viongozi wa Mila;***
- ***Waandishi wa habari;***
- ***Wananchi wa Mkoa wa Lindi;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

***Kazi na Utu…***

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania…***

Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa rehema zake ametuwezesha kukusanyika hapa kwenye Uwanja wa Ilulu tukiwa wazima na wenye afya kwa ajili ya maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani, na uzinduzi wa Kampeni za Upandaji Miti Kitaifa. Aidha, nashukuru uongozi wa Wizara ya Maliasili na Utalii, pamoja na Mkoa wa Lindi kwa maandalizi mazuri ya maadhimisho haya na kwa kunipa heshima kubwa ya kuwa Mgeni rasmi. Nawapongeza pia wananchi wa Lindi na wadau wengine kwa kujitokeza kwa wingi kushiriki katika maadhimisho haya. "***Hongereni Sana***."

Kabla sijaendelea, napenda kuwaletea salamu nyingi kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ni Mhifadhi Mkuu na Mwongoza watalii namba

moja nchini. Kupitia jitihada zake, sekta ndogo ya misitu na sekta yote ya utalii imekua na kuimarika, na kuifanya Tanzania kutambulika kimataifa kama kituo bora cha utalii duniani. Uthibitisho wa hatua hii kubwa iliyopigwa ni tuzo mbalimbali ambazo hivi karibuni nchi yetu imezipata kupitia taasisi na majukwaa mbalimbali duniani.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***
Leo Tanzania inaungana na Mataifa mengine Duniani kufanya maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani ikiwa ni hatua ya kutambua mchango wa misitu katika uhai wa mwanadamu na ukuaji wa uchumi kwa ujumla. Ni siku muhimu inayolenga kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa rasilimali misitu, na kutukumbusha kuhusu jukumu la kulinda misitu ili kuendeleza maisha ya mwanadamu hapa duniani. Katika siku hii, pia tunazindua rasmi ***Kampeni ya Upandaji Miti Kitaifa*** kama sehemu ya jitihada za kulinda na kuhifadhi rasilimali misitu, ambapo siku hii inatumika kuhimiza, kuelimisha na kuhamasisha Umma wa Watanzania kupanda na kutunza miti.

Kaulimbiu ya maadhimisho haya Kitaifa isemayo "***Misitu ni Uchumi Endelevu, Tuihifadhi kwa Maendeleo ya Taifa***.", na ile ya Kidunia "**Misitu na Uchumi**" (*Forests and Economies)* zote zinachagiza kutambua umuhimu wa misitu na mchango wake katika kukuza na kujenga uchumi wa nchi. Kaulimbiu ya kitaifa inaendana na mipango yetu ya Taifa, ikiwemo Dira 2050 pamoja na mikakati mingine yenye nia ya kuifanya Tanzania inufaike kupitia rasilimali za misitu, kwani misitu ina mchango mkubwa katika uhifadhi wa wanyamapori, ufugaji nyuki, utalii, kilimo, upatikanaji wa maji kwa matumizi nyumbani, viwandani na mashambani. Tanzania inakadiriwa kuwa na eneo la misitu lenye ukubwa wa takriban hekta milioni 48.1 sawa na 55% ya eneo lote la nchi kavu. Katika eneo hili, hekta milioni 44.7 (93%) ni misitu ya uoto wa miombo) na hekta milioni 3.4 (7%) ni Misitu ya Uwanda wa Chini, Milimani, Mikoko na Mashamba ya Miti. Sekta ya Misitu inayojumuisha ufugaji nyuki na wanyamapori, ilichangia takriban 3% katika Pato la Taifa mwaka 2024, hivyo kuifanya kuwa miongoni mwa vichocheo muhimu vya maendeleo ya Taifa. Kwa upana wake (i.e. ikijumuishwa mifumo ikolojia isiyothaminishwa na soko) misitu inakadiriwa kuchangia takriban 20% ya Pato la Taifa (*Green Accounting Study by TAFORI, 2025*).

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Pamoja na faida lukuki za rasilimali misitu, bado kuna changamoto nyingi zinazoikabili, zikiwemo: Utegemezi mkubwa wa rasilimali za misitu kwa uchumi na kipato kwa jamii kwa njia ya kuni, mkaa na mbao; idadi kubwa ya mifugo inayoingizwa katika hifadhi za misitu kwa ajili ya kutafuta malisho; matukio ya uvamizi wa hifadhi za misitu kwa shughuli za kibinadamu hususan makazi, kilimo na uchimbaji wa madini; pamoja na uwepo wa matukio ya moto ndani ya hifadhi za misitu. Changamoto hizi na nyinginezo zimesababisha kiwango cha upotevu wa misitu nchini kuongezeka hadi kufikia hekta 469,400 kwa mwaka. Hiki ni kiwango kikubwa sana kisichoweza kuendelea kuvumilika, na hivyo kututaka kushirikiana kuhakikisha misitu yetu inalindwa na kuhifadhiwa.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Kampeni ya upandaji miti kitaifa tunayoizindua leo ni sehemu ya jitihada za makusudi zinazochukuliwa ili kulinda hifadhi za misitu na kuongeza uwajibikaji katika uhifadhi wa mazingira yetu. Pia, ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2025 – 2030) ambayo inalenga kulinda rasilimali za ardhi, misitu, maji na viumbe hai kwa lengo la kutetea ustawi wa wananchi na ukuaji wa uchumi endelevu. Hivyo, ajenda ya upandaji miti, uhifadhi wa misitu na utunzaji wa mazingira kwa ujumla ni kipaumbele katika Taifa letu. Hii ni ajenda inayogusa makundi mbalimbali katika jamii kwa njia ya ukusanyaji na usambazaji wa mbegu za miti; ukulima wa miti; biashara ya mazao ya misitu; utoaji wa huduma za ugani katika mashamba ya miti na vitalu; na ushiriki katika mnyororo mzima wa mazao ya misitu.

Aidha, katika kukabiliana na changamoto za uhifadhi wa misitu, natambua jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali, Sekta binafsi na Wadau wa Maendeleo. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutenga na kuhifadhi kisheria maeneo ya misitu; kuhamasiha kampeni ya kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka kwa kila halmashauri; kuanzisha Kampeni ya Tanzania ya Kijani; kuanzisha mashamba mapya ya miti ya Serikali na ya watu binafsi; kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongoa ardhi ikiwemo programu ya *Africa Forest Landscape Restoration Initiative (*AFRI 100) yenye lengo la kurejesha eneo la hekta milioni 5.2 za misitu, ifikapo mwaka 2030 na, kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na biashara ya kaboni.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Mkoa wa Lindi ni miongoni mwa mikoa yenye rasilimali nyingi za misitu ya asili na mashamba ya miti, ambapo wananchi wake wanajishughulisha na kilimo, ufugaji na shughuli nyingine za kiuchumi zinazotegemea moja kwa moja mazingira. Mkoa huu pia una hazina kubwa ya misitu ya Miombo na Mikoko katika ukanda wa Pwani, ambavyo ni muhimu katika kulinda bioanuwai, vyanzo vya maji, na uchumi wa mazao ya misitu. Licha ya hivyo, taarifa zilizopo zinaonesha kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa hifadhi za misitu, hasa Mikoko, kutokana na kasi kubwa ya ukataji wa miti kwa shughuli za kilimo, na uchomaji moto wa mara kwa mara katika hifadhi za misitu. Hivyo, ninautaka uongozi wa mkoa wa Lindi kuhakikisha maeneo yote ya misitu yaliyohifadhiwa ndani ya Mkoa huu yanaendelea kulindwa na kutunzwa. Aidha, simamieni ili kuhakikisha vijiji vinakuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi ambayo inasimamiwa vema.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Kwa kutumia fursa ya Kilele cha Siku ya Misitu Duniani, napenda kuweka misisitizo katika masuala machache muhimu yahusuyo uhifadhi wa rasilimali misitu, kama ifuatavyo:

**Kwanza,** uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti kitaifa hapa Mkoani Lindi ni sehemu ya kutambua na kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais za kutunza mazingira. Kupitia kampeni ya upandaji miti ijulikanayo kama ***27 YA KIJANI,*** Mheshimiwa Rais ameonesha mfano na amekuwa kinara wa upandaji miti. Mathalan, aliposheherekea siku ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwake mwaka huu alipanda miti na kuhimiza Watanzania kufanya hivyo pia. Kwa taarifa nilizonazo, tangu kampeni hii ilipoanza mwaka 2023 jumla ya miti takriban 113,199,359 imepandwa katika maeneo mbalimbali nchini. Hivyo, hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Rais na kumuunga mkono kwa kuendelea kushiriki katika kupanda na kutunza miti.

Kama njia ya kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais, ninaelekeza Uongozi wa Mkoa wa Lindi na mikoa yote nchini kuhakikisha jitihada za upandaji miti zinaendelezwa kwa kuwekewa mkakati mahsusi unaojumuisha makundi yote katika jamii na kuzingatia ikolojia ya maeneo husika, ikiwa ni pamoja na kuzuia uvamizi/uharibifu wa maeneo yote ya hifadhi ya misitu.

**Pili,** ni muhimu kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi jirani na misitu ya asili na mashamba ya miti wanapatiwa elimu endelevu kuhusu matumizi bora ya ardhi, udhibiti wa uchomaji moto holela, na usimamizi shirikishi wa misitu ya vijiji. Nafahamu kwamba jitihada kubwa zimefanyika katika utoaji elimu na hamasa ili kujenga uadilifu katika matumizi ya rasilimali zetu. Lakini jitihada kubwa zaidi za pamoja zinahitajika katika utoaji elimu kuhusu kudhibiti uharibifu wa rasilimali zetu. Hivyo basi, angalieni uwezekano wa kuunganisha nguvu kati ya wadau, ili kuwa na programu kubwa zaidi za uelimishaji.

**Tatu,** Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI) inatakiwa kufanya tafiti zitakazojibu changamoto mbalimbali ambazo wakulima wa miti wanakabiliana nazo, hususan zile zinazojitokeza kwenye misitu yetu ya asili. Aidha, tafiti hizo zijumuishe zile zinazohusu miti inayofaa kwa maeneo ya Mkoa wa Lindi na mikoa mingine nchini, ikiwa ni pamoja miti dawa.

**Nne,** ni hitaji la kulifanya zoezi la upandaji miti kuwa endelevu. Ninaitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Mfuko wa Misitu (TaFF) kuwezesha miradi ya upandaji miti kwa kuanzisha mashamba ya miti ya vijiji na watu binafsi. Aidha, nautaka Wakala a Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuanzisha vitalu vya miche ya miti vya kutosha katika maeneo mbalimbali ya nchi, ikiwemo miti ya asili itakayopandwa katika maeneo mbalimbali. Sambamba na hilo, elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi ili kutunza na kukuza miti hiyo.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Kwa kumalizia, nawashukuru waandaaji na wote mlioshiriki katika maadhimisho haya yaliyofana. Naendelea kutoa rai kwa kila mwananchi kushiriki jitihada za kupanda miti na kuitunza.

Baada ya kusema hayo, nawatakia Maadhimisho mema ya Siku ya Kimataifa ya Misitu Duniani na Siku ya Upandaji Miti Kitaifa kwa mwaka 2026.

**Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika**
**Asanteni kwa kunisikiliza**